**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**687 VITENDO VYA KUJIFUNZA HAIBA NA MICHEZO**

**Muda: Saa 3.** **Alhamis 12 Mei 2016 mchana**

---

**Maelekezo.**

1. Karatasi hii ina sehemu **A** na **B** zenye jumla ya maswali **kumi na sita (16)**.
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu **A** na maswali **manne (4)** kutoka katika sehemu **B.**
3. Sehemu A ina alama **arobaini (40)** na sehemu B ina alama **sitini (60)**
4. Simu za mkononi na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **namba yako ya mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii

1. Bainisha mbinu nne za upimaji zinazofaa kutumika katika somo la Vitendo Vya Kujifunza Haiba na Michezo.
2. Eleza kwa kifupi dhana ya kujitambua na jinsi michezo inavyoweza kuisaidia. Toa hoja nne.
3. Fafanua kwa kifupi umuhimu wa nne wa kupanga darasa au eneo la kujifunzia kwa mtindo wa vituo vya kujifunzia.
4. Taja na ueleze kwa kifupi aina nne za adhabu mbadala ambazo hazijumuishi viboko.
5. Eleza umuhimu nne wa kujenga mahusiano mazuri kati ya mwalimu na mtoto katika kufundisha haiba.
6. Bainisha kwa kifupi zana nne za gharama nafuu ambazo mwalimu anaweza kutengeneza kwa kutumia vifaa vilivyotumika.
7. Fafanua kwa kifupi changamoto nne zinazoweza kutokea katika utekelezaji wa azimio la kazi lililoandaliwa vizuri.
8. Eleza kwa kifupi faida nne za kutumia nyimbo na mashairi katika kufundisha tabia njema na nidhamu.
9. Taja na ufafanue kwa kifupi mambo manne muhimu ya kuzingatia wakati wa kupanga muda wa kipindi cha michezo.
10. Eleza kwa kifupi jinsi nne ambazo michezo inaweza kumsaidia mtoto kukabiliana na hofu au soni.

## SEHEMU B (Alama 60)

Jibu maswali **manne (4)** katika sehemu hii

11. Kwa kutoa hoja tano fafanua jinsi uhuru wa mtoto katika michezo unavyochangia katika kukuza uwezo wake wa kufanya maamuzi.
12. Eleza kwa kina mbinu tano za kuzuia utovu wa nidhamu kabla haujatokea katika michezo.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

13. Jadili kwa hoja tano athari za kisaikolojia za kufanya mzaha au kumdhihaki mtoto mbele za wenzake.

14. Changanua kwa kina majukumu matano ya mwalimu katika kuhakikisha zana za michezo zinatumika ipasavyo na kwa usalama.

15. Maandalizi ya somo ni lazima yaakisi mahitaji ya wanafunzi wenye mahitaji maalum. Tetea kauli hii kwa hoja tano.

16. Eleza kwa hoja tano namna ya kuwafanya watoto wenye tabia za kujitenga washirikiane na wenzao katika michezo.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org